JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO



TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA WA KWANZA (NOVEMBA, 2015 – NOVEMBA, 2016)

SEKTA YA UJENZI

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi
na Mawasiliano (Ujenzi),
7 Barabara ya Samora Machel,
S.L.P 9423,
11475 Dar Es Salaam.
Baruapepe:ps@mow.go.tz

Novemba, 2016

TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA WA KWANZA - SEKTA YA UJENZI

1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali. Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo iliingia madarakani tarehe 5 Novemba, 2015 (Novemba, 2015 – Novemba, 2016), Wizara imetekeleza kwa mafanikio majukumu yake. Hii ni kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano kutoa fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya Wizara hasa kwa miradi ya maendeleo.

2.0 KAZI ZILIZOFANYIKA KUANZIA NOVEMBA, 2015 HADI NOVEMBA, 2016

2.1 MIRADI YA BARABARA

Utekelezaji wa miradi ya barabara katika kipindi cha kuanzia Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016 ni kama ifuatavyo:

a) Miradi ya Barabara na Madaraja Iliyokamilika - Kilometa 633 na Daraja Kubwa Moja (1)

(i) Ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Kwanza katika Jiji la Dar es Salaam (km 20.9); ujenzi umekamilika Desemba, 2015 na miundombinu hiyo imeanza kutumika Mei, 2016;

(ii) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni (Daraja la Nyerere) umekamilika Februari, 2016 na daraja limeanza kutumika;

(iii) Upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge kutoka njia tatu kuwa njia tano (km 4.3) umekamilika Julai, 2016;

(iv) Ujenzi wa Barabara ya Namtumbo – Tunduru (km 193);
- Sehemu ya Namtumbo - Kilimansera (km 60.7) umekamilika.
- Sehemu ya Matemanga – Tunduru (km 58.7) umekamilika.

(v) Ujenzi wa Barabara ya Tunduru – Mangaka – Mtambaswala (km 202.5)

- Sehemu ya Nakapanya – Tunduru (km 66.5) ujenzi umekamilika Septemba, 2016.
- Sehemu ya Mangaka – Mtambaswala (km 65.5) ujenzi umekamilika Agosti, 2016.
- Sehemu ya Mangaka – Nakapanya (km 70.5) umekamilika Septemba, 2016.

(vi) Ukarabati wa Barabara ya Mkumbara – Same (km 96) ujenzi umekamilika;

(vii) Ujenzi wa Barabara ya Lwanjilo – Chunya (km 36) ujenzi umekamilika;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi: Sehemu ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) umekamilika;

(ix) Ujenzi wa Barabara ya Nzega – Puge (km 58.8) umekamilika;

(x) Ujenzi wa Barabara ya Kawawa Roundabout – Msimbazi Twiga (km 2.7) umekamilika;

(xi) Ujenzi wa Barabara ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.6) umekamilika;

(xii) Ujenzi wa Barabara ya Kimara – Kilungule – External (km 3) umekamilika;

(xiii) Ujenzi wa Barabara ya Wazo Hill – Goba – Mbezi (km 7) umekamilika na;

(xiv) Ujenzi wa Barabara ya Tangibovu – Goba (km 9) umekamilika.

b) Miradi ya Barabara na Madaraja Ambayo Imetekelezwa kwa Asilimia Kubwa - Kilometa 979.6 na Madaraja Makubwa Mawili (2)

(i) Ujenzi wa Barabara ya Namtumbo – Tunduru (km 193); Sehemu ya Kilimansera – Matemanga (km 68.2); kuendeleza ujenzi ambapo kilometa 42.7 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(ii) Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Babati (km 261);
- Sehemu ya Dodoma – Mayamaya (km 43.65); kilometa 35.05 zimekamilika na ujenzi unaendelea.
- Sehemu ya Mela – Bonga (km 88.8); kilometa 44.34 zimekamilika na ujenzi unaendelea.
- Sehemu ya Mayamaya – Mela (km 99.35); kilometa 57.2 zimekamilika na ujenzi unaendelea.

(iii) Ujenzi wa Barabara ya Magole – Turiani (km 48) ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 69;

(iv) Ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64) ujenzi wa barabara umekamilika na ujenzi unaendelea kwa sehemu iliyobaki ya maingilio ya Daraja la Ruvu Chini;

(v) Ujenzi wa Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora; Sehemu ya Tabora - Nyahua (km 85); kilometa 78.33 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(vi) Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Urambo; Sehemu ya Ndono – Urambo (km 51.98); kilometa 50.8 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(vii) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Kanazi (km 75); ujenzi umekamilika kwa asilimia 69.39;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Usagara – Kisesa (km 17); ujenzi umekamilika kwa asilimia 65;

(ix) Ujenzi wa Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo: Sehemu ya Kyaka - Bugene (km 59.1); kilometa 57.0 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(x) Ujenzi wa Barabara ya Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) kilometa 39.67 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(xi) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 110); kilometa 66.00 zimekamilika na ujenzi unaendelea;

(xii) Ujenzi wa Daraja la Kilombero umekamilika kwa asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Desemba, 2016;

(xiii) Ujenzi wa Barabara ya Kaliua – Kazilambwa (km 56); kilometa 42 zimekamilika na ujenzi unaendelea na;

(xiv) Ujenzi wa Barabara ya Sitalike – Mpanda (km 36.9); umekamilika kwa asilimia 76 na ujenzi unaendelea.

c) Miradi ya Barabara Ambayo Utekelezaji wake Unaendelea – Kilometa 656.8, Madaraja Makubwa Mawili (2) na *Flyover/Interchange* Mbili (2)

(i) Ujenzi wa njia za juu katika makutano ya TAZARA; umeanza Februari, 2016 na ujenzi unaendelea;

(ii) Ujenzi wa Barabara ya Bunda – Kisorya (km 50); ujenzi unaendelea;

(iii) Ujenzi wa Barabara ya Uyovu – Bwanga (km 45); umetekelezwa kwa asilimia 40, ujenzi unaendelea;

(iv) Ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange); zabuni imetangazwa tarehe 20 Januari, 2016. Kwa sasa uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi upo katika hatua za mwisho;

(v) **Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander**: Mkataba kwa ajili ya usanifu wa kina, maandalizi ya nyaraka za zabuni na usimamizi wa ujenzi wa daraja umesainiwa Julai, 2016. Kazi za usanifu zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Januari, 2017.

(vi) **Ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze kwa Kiwango cha *Expressway* kwa Utaratibu wa Ubia Kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) - km 142:** Kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea. Mhandisi Mshauri amewasilisha rasimu ya taarifa ya upembuzi yakinifu ambayo kwa sasa inapitiwa ili kutoa maoni na hatimaye kuandaa taarifa ya mwisho ya upembuzi yakinifu wa mradi ambayo itatumika kumpata mwekezaji.

(vii) Ujenzi wa Daraja la Sibiti umekamilika kwa asilimia 22 na ujenzi unaendelea;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu: Sehemu ya Makutano – Natta (km 50) umekamilika kwa asilimia 33 na ujenzi unaendelea;

(ix) Ujenzi wa Barabara ya KIA – Mererani (km 26); umekamilika kwa asilimia 21.8 na ujenzi unaendelea;

(x) Ujenzi wa Barabara ya Bwanga – Biharamulo (km 67); umekamilika kwa asilimia 32.86 na ujenzi unaendelea;

(xi) Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (km 356): Sehemu ya Tabora – Sikonge (Usesula) (km 30); ujenzi unaendelea;

(xii) Ujenzi wa Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 268);

- Sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50); ujenzi unaendelea.
- Sehemu ya Kibondo – Nyakanazi (km 50); ujenzi unaendelea.

(xiii) Ujenzi wa Barabara ya Arusha – Holili: Sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na Arusha Bypass (km 42.4); umetekelezwa kwa asilimia 32.4.

(xiv) Ujenzi wa Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi: Sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50.3) unaendelea;

(xv) Ujenzi wa Barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema; Sehemu ya Tenende – Matema (km 34.6) unaendelea;

(xvi) Ujenzi wa Barabara ya Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6) unaendelea na;

(xvii) Upanuzi wa barabara ya Mwanza Mjini - Uwanja wa Ndege (km 2.8) pamoja na ujenzi wa Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha umekamilika kwa asilimia 57.

d) Miradi ya Barabara na Madaraja Ambayo Mikataba ya Ujenzi Imesainiwa/Inatarajiwa Kusainiwa - Kilometa 162.2 na Daraja Kubwa Moja (1)

(i) Ujenzi wa barabara ya Sanya Juu – Kamwanga (km 75), Sehemu ya Sanya Juu – Alerai (km 32.2);

(ii) Ujenzi wa barabara ya Mpanda – Usimbili (km 30), mkataba umesainiwa Julai, 2016;

(iii) Ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa (Sehemu ya Mawengi – Lusitu km 50), mkataba umesainiwa Agosti, 2016;

(iv) Ujenzi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (Sehemu ya Mtwara – Mnivata km 50);

(v) Ujenzi wa Daraja la Ruhuhu;

e) Miradi ya Barabara na Madaraja Ambayo Zabuni Zimetangazwa/Zinatarajiwa Kutangazwa - Kilometa 925.6, Madaraja Makubwa Matatu (3) na *Flyovers* Mbili (2)

(i) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Chunya - Makongolosi (km 43);

(ii) Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (BRT Phase II) ambayo itahusisha ujenzi wa barabara za Kilwa, Chang'ombe na sehemu ya barabara ya Kawawa zenye jumla ya

kilometa 20.3. Awamu hii ambayo itagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika itahusisha pia ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Chang'ombe na UHASIBU;

(iii) Ujenzi wa barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (Sehemu ya Usesula – Komanga km (108) na Sikonge Spur (km 7.5);

(iv) Ujenzi wa barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (Sehemu ya Komanga – Kasinde km (108) na Inyonga Spur (km 4.8);

(v) Ujenzi wa barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (Sehemu ya Kasinde – Mpanda km (108) na Urwira Spur (km 3.7);

(vi) Ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66);

(vii) Upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (Old Bagamoyo) – km 5.2 na Daraja la Mlalakuwa;

(viii) Upanuzi wa barabara ya Bendera Tatu – Kamata (km 1.3);

(ix) Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu (BRT Phase III) itakayohusisha barabara za Nyerere na Uhuru, Bibi Titi na Azikiwe kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto (km 23.6);

(x) Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi (km 3.2);

(xi) Ujenzi wa Daraja la Momba na;

(xii) Ujenzi wa Daraja la Sukuma;

(xiii) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mugumu – Natta (km 50);

(xiv) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Loliondo - Mto wa Mbu Sehemu ya Waso – Sale Junction (km 50);

(xv) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe - Makete (km 109):

- Njombe - Moronga (km 54.5)
- Moronga - Makete (km 54.5)

(xvi) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Uvinza - Mpanda (Sehemu ya Uvinza – Magunga: (km 60);

(xvii) Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Mkiwa - Itigi - Lulanga (km 57);

(xviii) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Urambo - Kaliua (km 28);

(xix) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpemba - Isongole (km 51) na;

(xx) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rudewa - Kilosa (km 18).

2.2 MASUALA YA USALAMA BARABARANI NA MIZANI YA KUPIMA UZITO WA MAGARI

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Tano, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za Usalama Barabarani kwa kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuweka Mfumo wa Taarifa za Ajali Barabarani (Road Accident Information System - RAIS)

Wizara imekamilisha kuweka mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ajali za barabarani, ambao utawezesha pamoja na masuala mengine, kupanga mikakati ya kutatua changamoto mbalimbali za usalama barabarani. Mfumo huo umeanza kutumika mwezi Agosti, 2016 kwa mikoa yote hapa nchini. Lengo la mfumo huo ni kupata idadi ya majeruhi, vifo na athari nyingine zinazotokana na ajali za barabarani. Mafunzo ya uingizaji wa taarifa za ajali za barabarani yanaendelea kutolewa kwa askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchi nzima.

(ii) Kuweka Mfumo wa Utoaji wa Vibali kwa Mizigo isiyo ya Kawaida kwa njia ya Kielektroniki (Electronic Abnormal Load Permit System)

Wizara imekamilisha uwekaji wa mfumo wa utoaji wa vibali kwa mizigo isiyo ya kawaida kwa njia ya kielekroniki. Mfumo huu umeanza kutumika mwezi Aprili, 2016 na unatekelezwa kwa kuwezesha vibali kutolewa kwa wakati na hivyo kupunguza muda kwa wasafirishaji kupata vibali hivyo.

(iii) Ufungaji wa Mizani Inayopima Magari Yakiwa Kwenye Mwendo (Weigh in Motion Weighbridges)

Mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo imejengwa katika eneo la Mikese, Morogoro. Mizani hii ni ya pili katika Ukanda wa Kati baada ya mizani ya Vigwaza Mkoani Pwani ambapo imesaidia kupunguza msongamano wa magari wakati wa kupima uzito na hivyo kupunguza kero ya kusubiri muda mrefu kwa wasafirishaji kupima magari.

(iv) Ufungaji wa Kamera za CCTV Kwenye Vituo vya Mizani ya Kupima Magari

Wizara inaendelea kuweka kamera za CCTV kwenye vituo vya mizani ili kuongeza uwazi na kuleta ufanisi wa utendaji kwenye vituo hivyo. Hivi sasa kamera hizo zimeshafungwa katika vituo vitatu vya Vigwaza, Horohoro na Sirari na ufungaji unaendelea kwenye vituo vingine nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa vituo vinafanya kazi kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa za kupima magari ya mizigo.

(v) Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi vya Pamoja (One Stop Inspection Stations - OSIS)

Ili kupunguza muda wa usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi, Wizara inaendelea na hatua za ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Stations – OSIS) katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam. Mradi wa ujenzi wa vituo vya ukaguzi vya pamoja katika eneo la Manyoni (Singida) na Nyakahura (Kagera) na upanuzi wa kituo cha Vigwaza (Pwani) katika Ukanda wa Kati upo katika hatua ya ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi. Aidha, mradi wa ujenzi wa vituo vya pamoja vya ukaguzi vya Mikumi (Morogoro), Makambako (Njombe) na Mpemba (Mbeya) katika Ukanda wa Dar es Salaam upo kwenye hatua ya usanifu. Lengo la kujenga vituo hivyo ni kupunguza vituo vya ukaguzi na hivyo kupunguza muda wa safari hususan kwa magari yanayosafirisha mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi za jirani katika kanda hizi.

Wizara imeanzisha utaratibu wa kutoa vibali maalum kwa magari yanayosafirisha mizigo nje ya nchi ili kuweza kupima uzito katika vituo vitatu ya mizani vya Vigwaza (Pwani), Njuki (Singida) na Nyakahura (Kagera) kwa magari yanayotumia Ukanda wa Kati. Aidha, kwa Ukanda wa Dar es Salaam, magari yanapimwa uzito katika vituo vinne vya mizani vya

Vigwaza (Pwani), Mikumi (Morogoro), Makambako (Njombe) na Mpemba (Mbeya).

2.3 MIRADI YA VIVUKO, NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI

2.3.1 Ununuzi na Ukarabati wa Vivuko

Serikali imeendelea na ununuzi wa vivuko vipya na ukarabati wa vivuko vilivyopo ili kuboresha huduma ya vivuko. Katika kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016, miradi ifuatayo imetekelezwa:-

(i) Wizara imekamilisha ujenzi wa Kivuko kipya cha Mto Pangani (MV Tanga) mkoani Tanga chenye uwezo wa kubeba tani 50 sawa na abiria **100** na magari **6**.

(ii) Ukarabati wa kivuko cha MV Magogoni chenye uwezo wa kubeba tani **500;** yaani abiria **2,000** na magari **60**, umekamilika**.**

(iii) Wizara imekamilisha ukarabati mkubwa wa kivuko cha MV Nyerere chenye uwezo wa kubeba tani 25 sawa na abiria 100 na magari mawili. Kivuko hicho kinatoa huduma kati ya Bugolora (Ukerewe) na Kisiwa cha Ukara mkoani Mwanza.

(iv) Kukamilisha ukarabati wa kivuko cha MV Kilombero II ambacho kilipata ajali ya kuzama majini katika Mto Kilombero mwezi Januari, 2016.

(v) Wizara inaendelea na ujenzi wa Kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni chenye uwezo wa kubeba tani 170 (sawa na abiria **800** na magari **22**). Kazi ya ujenzi wa kivuko hiki ilianza rasmi tarehe 01 Juni, 2016 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2016.

(vi) Taratibu za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi chenye uwezo wa kubeba tani **250** (sawa naabiria **1,000** na magari **46**) unaendelea.

(vii) Wizara inaendelea na taratibu za zabuni kwa ajili kupata Makandarasi wa kujenga na kuleta boti tatu (3) za kivuko cha Utete, Kilambo na Pangani.

(viii) Kuendelea na taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kufanya kazi ya kuhuisha mashine za kukatia tiketi (automated vending machine) kwa ajili ya kuboresha mapato katika kivuko cha Magogoni – Kigamboni.

2.3.2 Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali

Katika kipindi cha Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016, Wizara imeendelea kutekeleza kazi za ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali pamoja na huduma ya ushauri kwa Wizara, Idara na Taasisi za Umma kuhusu miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali. Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Jengo la ghorofa 10 lililopo Mtaa wa Wachaga, Arusha ulikamilika Novemba, 2015

(ii) Ujenzi wa Jengo la ghorofa 8 lililopo eneo la Ada Estate (Dar es Salaam) ulikamilika Februari, 2016.

(iii) Ujenzi wa nyumba 8 za Majaji katika mikoa ya Arusha (1), Tanga (1), Dar es Salaam (2), Mbeya (1), Iringa (1), Dodoma (1) na Ruvuma (1) umekamilika Januari, 2016.

(iv) Ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Umma eneo la Bunju – Dar es Salaam Awamu ya Pili (Nyumba 128) unaendelea. Aidha, TBA inaendelea na ukamilishaji wa nyumba za Majaji na nyumba za Watumishi wa Umma mkoani Pwani.

(v) Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) umekamilisha ujenzi wa karakana mpya ya matengenezo ya magari mkoani Manyara mwezi Novemba, 2015.

(vi) Kuanza ujenzi wa majengo yenye ghorofa 8 eneo la Magomeni *Quarters* Mkoani Dar es Salaam yenye jumla ya nyumba **644** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 20.0**

(vii) Wakala wa Majengo Tanzania unaendelea na ujenzi wa madarasa, mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shule za Sekondari yenye thamani ya **Shilingi bilioni 35.6** kama ifuatavyo:-

a) Ujenzi wa mabweni **20** ya Wanachuo wa Chuo Kikuu cha DSM sehemu ya Mlimani kwa gharama ya Shilingi **bilioni 10.0**.

b) Ujenzi wa mabweni **12** na madarasa **6** na nyumba **30** za walimu wa shule ya Sekondari Ihungo na ukarabati wa majengo ya maabara yaliyoharibiwa na tetemeko la ardhi mkoani Kagera.

c) Ujenzi wa mabweni **12,** madarasa **6**, nyumba **25** za walimu na jengo **1** la Utawala katika shule ya Sekondari Nyakato mkoani Kagera.

d) Ujenzi wa nyumba **20** za walimu katika shule ya Sekondari Rugambwa zilizoharibiwa na tetemeko la ardhi mkoani Kagera.

(viii) Ukarabati wa nyumba na majengo 24 kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 6.0** umetekelezwa kama ifuatavyo:-

a) Ukarabati wa majengo **14** ya Ikulu Ndogo ya Chamwino.
b) Ukarabati wa majengo matatu **(3)** ya Ikulu Ndogo ya Arusha
c) Ujenzi wa majengo **7** ya Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma.
d) Ukarabati wa nyumba **27** za Viongozi zilizopo maeneo ya Msasani, Kijitonyama na Mikocheni.
e) Ukarabati wa majengo **61** ya Wakala wa Majengo (TBA) nchi nzima.

(ix) Kununua jumla ya viwanja **22** vyenye ukubwa wa hekari **3.5.**

(x) Kuhusu Ajira na Mafunzo ya Watumishi, Wakala wa Majengo umetekeleza yafuatayo:-

a) Kutoa ajira **2,060** za mafundi na vibarua wa kutekeleza miradi mbalimbali nchi nzima ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali.
b) Kutoa mafunzo kwa wanafunzi **62** walio katika mafunzo kwa vitendo kutoka katika Vyuo Vikuu vitano (5).
c) Kutoa mafunzo kwa Wahitimu **42** wa Vyuo Vikuu ili kupata usajili wa Bodi za Kitaaluma (AQRB na ERB).

(xi) Uanzishwaji wa Kikosi cha Ujenzi Tanzania (Tanzania Building Agency – Brigade) kumewezesha kupunguza gharama za ujenzi kwa asilimia kati ya 30 na 40.

(xii) Ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majengo bila kuyaharibu/ kuyabomoa (Non - Destructive Testing – NDT Equipment) vinavyopima ubora wa majengo kwa haraka. Vifaa hivyo ni:-

a) *Rebound Hammer* kwa ajili ya kupima uimara wa zege lililokauka.
b) *Concrete cover meter/ Rebar locator* kwa ajili ya kupima ukubwa wa nondo na umbali uliowekwa.
c) *Ultrasonic System/Testing Device* kwa ajili ya kupima muonekano wa ndani wa zege lililokauka.

2.4 UJENZI NA UKARABATI VIWANJA VYA NDEGE

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani Novemba, 2015, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ya ujenzi, ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja ni kama ifuatavyo:-

i) Kukamilika kwa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma mwezi Agosti, 2016;
ii) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria (TB II) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Hivi sasa majadiliano kuhusu Mkataba wa Mkopo baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufaransa yanaendelea;
iii) Kukabidhi eneo la mradi kwa Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya viungio, eneo la maegesho ya ndege na ujenzi wa mifumo ya taa za kuongozea ndege. Kuweka mifumo ya mawasiliano ya kuongozea ndege (NavAids) katika Kiwanja cha Ndege Tabora mnamo mwezi Agosti, 2016;
iv) Kazi ya ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza unaendelea;
v) Kuanza kazi ya kusimika taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege Songwe Septemba, 2016;
vi) Kukamilika usanifu wa kina na kufanya maandalizi ya makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara.
vii) Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (TB III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambalo limekamilika kwa asilimia 65;
viii) Wizara inaendelea na ununuzi wa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma awamu ya pili.
ix) Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora awamu ya pili umeanza Agosti, 2016;
x) Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege 11 umekamilika mwezi Oktoba, 2016. Viwanja hivyo ni Lindi, Iringa, Njombe, Musoma, Moshi, Tanga, Songea, Singida, Lake Manyara, Kilwa Masoko na Simiyu;
xi) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Geita unaendelea.
xii) Taratibu za zabuni kwa ajili ya kuwapata Makandarasi wa kufanya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga na Shinyanga zipo katika hatua za mwisho; na

xiii) Maandalizi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Mtwara, Musoma, Iringa na Songea yameanza.

2.5 USIMAMIZI NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Katika kipindi cha kuanzia Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016 Wizara imeendelea kuimarisha uwajibikaji katika usimamizi wa Rasilimali Watu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Maadili na Misingi ya Utumishi wa Umma. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kufanya uhakiki wa Rasilimali Watu pamoja na taarifa za malipo ya mishahara (Computer Processed Payroll Data Sheet) kwa watumishi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98 –Ujenzi) na Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya udhibiti wa taarifa za kiutumishi na malipo ya mishahara;

(ii) Kupitia vyeti vya Kitaaluma (Kidato cha Nne na Sita) na Mafunzo (Vyuo) vya watumishi wote na kuwasilisha Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) kwa ajili ya uhakiki ili kubaini watumishi ambao wamejipatia ajira kwa njia ya udanganyifu;

(iii) Kusimamia ajira ya raia wa kigeni wanaofanya kazi katika miradi ya barabara na madaraja ili kudhibiti na kuepuka ajira holela ya wageni katika miradi ya umma na;

(iv) Kufanya maandalizi ya kuhamia Dodoma. Utekelezaji wa Agizo la kuhamia Dodoma unazingatia maelekezo ya Serikali ambapo unafanyika kwa Awamu 3. Awamu ya Kwanza inawahusu Viongozi Wakuu wa Wizara na Menejimenti ambao watahamia kati ya mwezi Septemba, 2016 na Februari, 2017. Awamu ya pili itakuwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Awamu ya Tatu katika mwaka wa fedha 2018/2019.

- Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imepata jengo la ghorofa tano (5) linalomilikiwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambalo litakuwa Makao Makuu ya muda ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Jengo hilo lipo katika hatua za mwisho za ujenzi (finishing). Wakala wa Majengo Tanzania unaendelea kukamilisha jengo hilo ikiwa ni pamoja na uwekaji umeme na maji, miundombinu ya mawasiliano na kutenganisha

(partitioning) vyumba kwa ajili ya Ofisi.

- Katika Mpango wa muda mrefu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) imeelekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuanza ujenzi wa nyumba hamsini (50) za makazi ya watumishi wa Serikali mjini Dodoma kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

3.0 FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (UJENZI)

Katika kipindi cha Novemba, 2015 hadi Oktoba, 2016 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipokea jumla ya **Shilingi 1,520,787,184,489.72** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha kiasi cha **Shilingi 485,064,900,380.00** fedha za Mfuko wa Barabara, **Shilingi 827,242,841,663.72** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 208,479,442,446.00** fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, bajeti ya miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,176,204,557,000.00.** Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 1,248,721,422,000.00,** fedha za nje ni **Shilingi 344,838,635,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara ni **Shilingi 582,644,500,000.00** ikilinganishwa na **Shilingi 883,832,338,500.00** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/16. Hii ni ongezeko la asilimia **146.22** ukilinganisha bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/17 na mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imetengewa **Shilingi bilioni 200** kwa ajili ya miradi ya viwanja vya ndege**.**

4.0 HITIMISHO

Katika mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016 kasi ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali imeongezeka kufuatia Sekta ya Ujenzi kupatiwa jumla ya **Shilingi 1,520,787,184,489.72** zinazojumuisha **Shilingi 827,242,841,663.72** fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, **Shilingi 208,479,442,446.00** fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 485,064,900,380.00** fedha za Mfuko wa Barabara. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) itaendelea kutekeleza kikamilifu majukumu yake hususan miradi ya maendeleo kulingana na mpango kazi na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.